2. Je! Paulo anamaanisha nini katika aya ya 7?
3. Je! Paulo alisema Maandiko Matakatifu yalipeanwa kwa nini? Mstari wa 16, 17.
4. Je! Wengine watafanya nini katika nyakati za mwisho? 1Timotheo 4: 1.
5. Vipi kuhusu dhamiri zao? Mstari wa 2.
6. Je! Imesemwa nini kuhusu matajiri wa siku za mwisho? Yakobo 5: 1-3.
7. Tuambie kwa nini matajiri watalia? Mstari wa 4.
8. Kando na kuishi katika raha za hapa duniani, wamefanya nini ingine? Mstari wa 6.
9. Katika nyakati hizi za hatari, Yahshua alisema tunapaswa kujitahadhari na nini? Luka 21:34, 35. Paulo alisema tunapaswa kufanya nini? Waebrania 10:25.
10. Je! Watu wa ulimwengu watakuwa na hisia gani wakati Mwana wa Mtu atakapokuja katika utukufu wake? Mathayo 24:30,

    **Maelezo**. Ni dhahiri kutoka kwa ishara zinazotuhusu kwamba tunaishi katika siku za mwisho. Nyakati za hatari ziko hapa na inafaa kila mmoja wetu kuinua vichwa vyetu kwa sababu ukombozi wetu unakaribia (Luka 21:28); Pia, kujishughulisha na kazi ya Baba yetu, kama watumishi wenye faida. Yohana 4:35, 36.

*******************************



8. Yerusalemu ilikuwa ijengwe upya wakati wa amani au shida? Danieli 9:25[sehemu ya mwisho].
9. Ni nini ilikuwa itokee kwa Masihi baada ya majuma sitini na mawili pamoja na wiki saba za kwanza, kwa jumla wiki 69? Danieli 9:26 [sehemu ya kwanza].
10. Ni nani alikuwa afuate baada ya Masihi? Alikuwa afanye nini? Danieli 9:26 [sehemu ya mwisho].

    **Maelezo**: Huyu alikuwa Tito kamanda wa majeshi ya Kirumi ambaye aliuteka mji wa Jerusalem katika mwaka wa 70 A.D, na kuharibu mji na hekalu kabisa.

11. Ni nini ilikuwa itokee katikati ya wiki hii ya mwisho ambayo ni wiki ya 70? Danieli 9:27 [sehemu ya kwanza].

    **Maelezo**: Hii ilikuwa kukatiliwa mbali, au kusulubiwa kwa Masihi, tukio ambalo lilileta rasmi mwisho, lengo na haja ya sheria ya msamaha kwa damu ya "kondoo ya dhabihu" na kuleta kipindi kipya cha neema.
12. Ni nini ilikuwa itokee baada ya kusulubiwa, kuhusiana na chukizo la uharibifu? Danieli 9:27 [sehemu ya mwisho]. Mwisho wa ukiwa ulikuwa hadi lini?

*******************************





***"Utakieni Yerusalemu amani; Na wafanikiwe wakupendao" Zaburi 122:6***



# Masomo Ya Bibilia

***kwa***

**KANISA LA ELOHIM (COG)**
**Siku Ya Saba (7th day)**

Robo Ya Kwanza
2023

Ya
Januari, Februari, Machi.
**(Tevet, Shevat, Adar, Nisan)**

Watenda kazi wanahitajika,
Mavuno ni mengi, lakini watenda kazi ni wachache...

**Tuma maombi yote kwa S.L.P 568, Jerusalem — Israel**

**Somo la Januari 28, 2023 (Shevat 6, 5783).**

## HALI ILIVYOTABIRIWA KATIKA SIKU ZA MWISHO

**Somo Kuu: 2 Timotheo 3**
**Fungu La Kukariri: 2 Timotheo 3:13.**

1. Je! Ni hali gani au nyakati zipi kwa ujumla zitatawala katika “Siku za mwisho?” 2 Timotheo 3:1.
2. Tamaa na ubinafsi zitakuwaje katika nyakati za siku hizo? 2 Timotheo 3:2.
3. Watu watakuwa wapenda anasa katika kipindi hicho? 2 Timotheo 3:4.
4. Je, kutakuwa na watauwa wengi wa dini na wamasihi wajifanyao halisi? 2 Timotheo 3:5.
5. Kutakuwa na kujifunza kwingi kwa wakati huu, ni wengi wataufikia ujuzi wa kweli? 2 Timotheo 3:7.
6. Hali ya dunia itaendelea kuwa bora au mbaya zaidi baada ya mtume kutoa huu unabii? 2 Timotheo 3:13.
7. Je! Mtume Yakobo anatujulisha nini kuhusu utajiri na mali katika siku za mwisho? Yakobo 5:1-3.
8. Isaya alitabiri nini kuhusu sheria na neno kutoka Yerusalemu katika siku za mwisho? Isaya 2:2, 3.



3. Je! Hukumu ya mwisho inamaanisha kuharibiwa kabisa kwa waovu? Malaki 4: 1-3
4. Je, ni vipi kuhusu wafu waovu waliokufa? Yohana 5: 28,29
5. Je! Ni nini itakuwa hatima ya wenye dhambi wote? Ufunuo 20: 15,21: 8
6. Je, ni faida kwetu kujua kuhusu hukumu inayosubiri? 2 Petro 3:17
7. Ni nafasi gani maalum ambayo mitume kumi na wawili watachukua wakati wa hukumu hii? Mathayo 19:28.
8. Je, wengine, kando na mitume kumi na wawili watachukua nafasi za mamlaka na hukumu? Ufunuo 20: 4-6; 26, 27.
9. Ni nani atakuwa Mfalme? Atatawala kwa muda gani? 1 Wakor. 5: 22-26
10. Tunapaswa kufanya nini ili kuhesabiwa kama moja ya kondoo wake na kuepuka moto wa milele? Mathayo 25: 31-41.

*******************************

**Somo la Machi 4, 2023 (Adar 11, 5783).**

## NYAKATI ZA HATARI

**Somo Kuu: 2 Timotheo 3.**
**Fungu La Kukariri: 2 Timotheo 3:14.**

1. Fafanua nyakati za hatari ambazo Paulo alinena kuzihusu? 2Timotheo 3: 1-7.



**Somo la Januari 7, 2023 (Tevet 14, 5783).**

## UNABII, MWANGA KATIKA ULIMWENGU WA GIZA

**Somo kuu: 2 Petro 1.**
**Fungu la kukariri: 2 Petro 1:21.**

1. Jinsi gani maandiko matakatifu yalitolewa? 2 Timotheo 3:16.
2. Je! Yalitolewa kwa malengo gani? 2 Timotheo 3:17.
3. Yaliyotabiriwa kwenye biblia yanatuongoza katika maisha ya sasa? Yatafanyaje? Kumbukumbu la Torati 29:29.

   **Maelezo**: Asilimia kubwa ya maneno ya biblia ni unabii. Yaliyoyatabiriwa kitambo yanahusu leo kabla tu ya “kuja kwake Masihi kwa mara ya pili”. Hata hivyo matumaini yetu na imani yetu kwa Baba yetu wa mbinguni na Yahshua, mwanawe, ni unabii - ufufuko wa wafu; uzima wa milele; hata kutangazwa na malaika wakati wa kuzaliwa kwake, “amani duniani na nia njema kwa watu wote” hata hivo hakuna cha kudhuru wala kuharibu. Hapatakuwa na mateso, maombolezo au huzuni – hakutakuwa na kifo wala maumivu. Haya ndiyo matamanio na matumaini yetu, yote ni unabii.



8. Bwana atakuja mahali gani atakaporudi duniani? Zek. 14:4
9. Ni nani atakayekuwa Mfalme wa ulimwengu wote wakati huu na baadaye? Zek. 14:9; Ufu. 11:15.
10. Je! Ni nini kilichosemwa zaidi kuhusu Makao Makuu ya Ufalme Wake? Je, kutakuwa na ongezeko la amani wakati huu? Zaburi 110:1-6; Isaya 9:6, 7.
11. Bwana na Mwokozi Yahshua Masihi atatawala akiwa Mfalme kwa muda gani? Ufu.20:4.

*******************************

Lakini sanamu ya Ufunuo 13:15 itakuwa na uwezo wa kufanya matangazo yake.

9. Je nguvu za shetani zilizaa uhai kabla ya siku za huyu mnyama? Kutoka 7: 11, 12; 8:7.
10. Ni kwa njia gani wote waliojiingiza kwenye nguvu za huu uovu watafahamika? Ufunuo 13:16.
11. Je, ni hatima gani inayowangoja wale wanaoishi katika utawala wa mnyama na wale wanaokataa kumwabudu? Ufunuo 13:15, 17.
12. Jinsi gani huyu mnyama atatambulika? Ufunuo 13:18.
13. Je, nguvu hizi ovu zitakuwepo wakati Yahshua atarudi katika dunia? Ufunuo19:11, 14, 19.
14. Je, mwisho wa mnyama huyu utakuwa upi? Ufunuo 19:20.

*******************************

**Somo la Februari 25, 2023 (Adar 4, 5783).**

## HUKUMU

**Somo Kuu: 2 Petro 3: 1-18**
**Fungu La Kukariri: 2 Petro 3:18**

1. Je! Kuna wakati uliowekwa wa hukumu? Matendo 17:31
2. Je, ni miji ipi miwili iliyowekwa kama mfano wa hukumu? 2 Petro 2: 6



9. Naye nabii Mika pia alitabiri nini kuhusu tukio hili katika siku za mwisho? Mika 4:1, 2.
10. Kufuatia matukio haya, nini itafanyika huko Yerusalemu wakati Masihi atakaporudi kuleta hukumu? Mika 4:3.
11. Ni nini kilichosemwa kuhusu siku za mwisho au "wakati wa mwisho," kuhusu ongezeko la maarifa? Danieli 12:4.
12. Ni kwa muda gani Kitabu cha Danieli kitakuwa kimefungwa na kutiwa muhuri, na wakati kitafunguliwa wazi, nani atakuwa na hamu yake, nani ambaye hatakuwa na hamu yake? Danieli 12:9, 10.

**Maelezo**: Kitabu cha Danieli bado kimefungwa na kutiwa muhuri kwa Israeli, na Wayahudi kwa ujumla. Laana imewekwa na Wayahudi waliokithiri (Orthodox Jews), juu ya mtu yeyote ambaye atakayetafsiri na kuhesabu Majuma 70 ya sura ya 9.

13. Ni nini kilichosemwa kuhusu njia za usafiri katika wakati wa maandalizi? Nahumu 2:3, 4.

**Maelezo**: Tunaishi katika wakati wa maandalizi kwa ajili ya mfalme ajaye, na hali hizi zinadhihirika kila mahali. Kila mwanaume na mwanamke ambaye ameitwa kutoka dunia, na anaelewa mambo haya, lazima awe mtumishi mwenye faida na katika kushuhudia na kwa



**Somo la Machi 25, 2023 (Nisan 3, 5783).**

## MFALME AJAYE, UFALME WAKE

**Somo Kuu: Ufunuo 20:1-6; Isaya 11:1-9**
**Fungu La Kukariri: Luka 12:32**

1. Je! mbingu zitamzuia Bwana na Mwokozi wetu Yahshua Masihi hadi lini? Matendo 3:20, 21.

**Maelezo**. "Nyakati za Kurejeshwa" haimaanishi wakati wa Kuangamizwa kwa kila kitu kilicho hai, bali ni urejesho wa ulimwengu mzima kurudi kwenye Paradiso ya Edeni; ilivyokuwa kabla mwanadamu hajatenda dhambi. Mwanzo 8:21.

2. Atakaporudi Bwana wetu atakuja na nini pamoja naye? Ufu. 22:12; Isaya 62:11.
3. Ufalme huo wa utakatifu utaendelea hadi lini? Danieli. 7:13, 14
4. Ufalme huo utakuwa wapi na utapewa nani? Danieli 7:27
5. Huyu "Binti Sayuni" analinganishwa na nini? Yeremia 6:2; Ufu. 19:7, 8
6. Mwanamke huyu, mfano wa kanisa la kweli, anaelezewa wapi kwa uhakika zaidi? Ufu. 12:1
7. Je! Ni nini kilichosemwa kuhusu imani ya kanisa hili la Mabaki? Ufu. 12:17.



4. Kitabu cha mwisho cha biblia kinaitwaje? Ufunuo 1:1.
5. Ni nini kimewekewa kwa wale watakaosoma unabii huu? Ufunuo 1:3.
6. Jinsi gani unabii wa agano la kale ulitolewa? 2 Petro 1:21.
7. Je! Nini kilichosemwa juu ya tafsiri ya unabii huu? 2 Petro 1:20.
8. Je, unabii huu unauhusiano wowote na unabii wa wokovu? 1 Petro 1:9-10.
9. Je, roho wa Masihi ana uhusiano wowote na manabii? 1 Petro 1:11-13.
10. Ni kwa jinsi gani Masihi mwana wa Elohim aliye hai alifunuliwa kwa Petro? 2 Petro 1:16, 17.
11. Ni kwa njia gani ya ajabu uwepo wake ulifunuliwa kwa Petro, Yakobo, and Yohana? 2 Petro 1:18; Mathayo 17:1-9
12. Ni kwa jinsi gani tutahuchukulia unabii huu wa ajabu kwa siku hizi na wakati huu wa sasa tunapoishi? 1 Kor 10:11; Warumi 15:4.
13. Petro, Yakobo, na Yohana, walipokea ufunuo wa kuja kwa Yahshua mara ya pili walipokuwa juu ya mlima mtakatifu. Lakini tuna nini hata leo juu ya kuja kwa Yahshua Masihi kwa mara ya pili? 2 Petro 1:19.

kujitolea maisha yake, katika zaka na sadaka, kuchapisha ujumbe huu, kuutuma kupitia wahudumu na wafanyakazi kwa Israeli, na kwa ulimwengu wa Mataifa.

*******************************

**Somo la Februari 4, 2023 (Shevat 13, 5783).**

## ISHARA ZA NYAKATI

**Somo kuu: Matayo 24:7-27.**
**Fungu la kukariri: 2 Timotheo 3:1.**

**MAELEZO**: Kuna unabii mwingi sana katika biblia unaozungumzia siku za mwisho. Tunaambiwa tukeshe na kuomba mambo haya yasitujie kama vile mwizi huja usiku. Bibilia inasema kwamba hakuna ajuaye siku au saa ya kuja kwake Mwokozi, hata hivyo tumepewa ishara nyingi za kutufanya tuwe tayari katika siku tunazoishi, siku za mwisho. Hebu tuone mambo waziwazi yaliyo nakiliwa kwenye biblia kwa ajili yetu, siku za zamani, za sasa na siku zijazo.

1. **KUSHUKA KWA ROHO MTAKATIFU** Matendo 2:17, soma pia Marko 16:17.
2. **KUACHA IMANI NA MAFUNDISHO YA UONGO** 1 Timotheo 4:1.
3. **KUTOAMINI NA WANAODHIHAKI**. 2 Petro 3:3.
4. **WADANGANYI WAKUU**. Mathayo 24:24.



linapotajwa kwenye maandiko matakatifu jinsia ya kike hutumika.

3. Wakati mnyama anatawala nani atafanya kazi naye? Ufunuo 19:20.
4. Je, ni matukio gani ya miujiza ambayo shetani ataonesha kwa nguvu zake? Ufunuo 13: 13, 14
5. Je, Yahshua alisema nini juu ya nguvu za shetani zitakazokuwepo kabla ya kuja kwake kwa mara ya pili? Mathayo 24: 2
6. Jinsi gani mtume Paulo alielezea yule mwovu, na alisema nini kuhusu nguvu za kishetani atakazomiliki? 2 Wathesalonike 2: 8-10.
7. Wakati wa utawala wa nguvu za yule mwovu, ni mamlaka gani atatumia kwa watakaoishi kwenye utawala wake? Ni nani ambaye watalazimishwa kumwabudu? Ufunuo 13: 12.

**Maelezo**: Tunaona kuwa huyu mnyama aliyeongozwa na Shetani atatumia nguvu za mnyama wa kwanza, kwake yeye lile kanisa liloanguka lilipanda.

8. Je, ni nguvu gani ya ajabu nabii wa uongo atamiliki ambaye hufanya kazi pamoja na mnyama? Ufunuo 13: 15.

**Maelezo**: Nebukadineza aliamuru sanamu itengenezwe katika wakati wa Danieli. Lakini sanamu ile ilikuwa haina uhai wala haiongei.



14. Je, mtu aliyeteuliwa kwa kweli, akaitwa kwa uzima wa milele, atapata mazao au hatapata mazao katika kazi ya Elohim kwa kipindi hiki? 2 Petro 1:8.

*******************************

**Somo la Januari 14, 2023 (Tevet 21, 5783).**

## UNABII WA KUJA KWA MASIHI

**Somo Kuu: Isaya 53.**
**Fungu La Kukariri: Luka 18:31.**

1. Musa alizungumza juu ya Masihi kwa maneno gani? Kumbukumbu la Torati 18:15.
2. Je! Tutawezaje kujua kwamba nabii aliyenenwa na Musa ndiye Masihi? Matendo 3:20-24.
3. Je! Nabii Isaya alitabiri juu ya ishara gani ya ajabu? Isaya 7:14.
4. Je, unabii huo ulitimizwa? Luka 1:26-31; 2:7; Mathayo 1:22, 23.
5. Kulingana na Mika, Masihi angezaliwa wapi? Mika 5:2.
6. Je, unabii huo ulitimizwa? Mathayo 2:1.
7. Ni unabii gani kumhusu Yahshua unaopatikana katika Hosea? Hosea 11:1.
8. Je, hili lilitimizwa? Mathayo 2:18, 14, 19-23.
9. Je! Kuja kwa Masihi kungetangazwaje? Isaya 40:3.



1. Katika Isaya sura ya 1-8, nabii anasimulia uzoefu mzuri. Je! Unaona chochote ndani yake ambacho kinaweza kuwa mfano kwetu katika zama hizi?
2. Je, Isaya alitabiri kuhusu kuzaliwa kwa Masihi? Isaya 9:6, 7; 11:1-5.
3. Ni kwa nini watu hawakujua Yahshua kama Masihi kupitia maarifa ya unabii huu, na wa manabii wengine? Isaya 6: 9-12.
4. Je! Isaya 53:1-3 inahusiana vyovyote na wazo hili?

**Maelezo**. Isaya 53 ni unabii wa kipekee wa Masihi. Kwa ufupi lakini kwa uzuri hutoa jumla ya kazi Yake kama Mwokozi wetu, unabii kuhusu kukataliwa kwake na watu na mateso yake kwa kuzibeba dhambi zetu. Kusoma sura hii moja inapaswa kuwashawishi wale walio na shaka.

5. Jadili Isaya 53: 10-12.
6. Mstari wa 8 ulitimizwaje hasa?

**Maelezo**. - Kulingana na mapokeo ya Rabbi, Isaya aliuawa akiwa na umri wa miaka 90, kutokana na amri ya Manase. Alikatwa vipande viwili kwa msumeno katika shina la mti. Inaaminiwa na baadhi ya wengine kuwa Waebrania 11:37 inahusu kifo chake.

*******************************

**Maelezo**: Hebu sasa tulinganishe tena Danieli na ufunuo. Urefu wa wakati (miezi 42 katika mstari wa 5) kwamba mnyama wa Ufunuo angekuwa na uwezo juu ya watakatifu, pia ni sawa na "nyakati na nusu wakati" ya Danieli 7:25.

11. Ni nini kilichosemwa kuhusu mnyama huyu ambaye anatawala chini ya kichwa kimoja, kujeruhiwa kwa upanga? Alipona jeraha la kifo? Ufunuo 13:3, 12-18.

*******************************

**Somo la Februari 18, 2023 (Shevat 27, 5783).**

## ALAMA YA MNYAMA

**Somo kuu: Ufunuo: 14:9-20.**
**Fungu la kukariri: Ufunuo 19:20.**

1. Kulingana na Danieli mnyama anaashiria nini katika unabii wa neno la Elohim? Danieli 7:17.
2. Je, baadhi ya sifa za mnyama zilizotajwa katika Ufunuo 13:11, ni gani?

   **Maelezo**: Wafalme wasiomcha Elohim au watawala wanasimamia mnyama katika maandiko matakatifu. Naomba ukumbuke kila wakati biblia inapoongea kuhusu mnyama, jinsia ya kiume ndio inayotumika. Popote kanisa



5. **MAJANGA KATIKA DUNIA**. Luka 21:11 soma pia Mathayo 24:7.
6. **NYAKATI NGUMU DUNIANI**. 2 Timotheo 3:1.
7. **KUZALIWA UPYA KWA ISRAELI**. Mika 4:1 soma pia Yeremia 29:14.
8. **KUBADILIKA KWA MAUMBILE**. Luka 21:25.
9. **ROHO YA MPINGA MASIHI**. 2 Thesalonike 2:9 soma pia 1 Yohana 4:3 na 2 Yohana 1:7.
10. Tutajua muda wa kuja kwake? Matendo 1:7.
11. Ni nini kimeahidiwa kwa wale wanaopokea na kuyashika maneno ya kinabii na ahadi zilizo ndani yake? ufunuo 1:3.
12. Je! Ni ujumbe upi uliopeanwa kwa dunia katika siku hizi za mwisho? Marko 1:15.

*******************************

**Somo La Februari 11, 2023 (Shevat 20, 5783).**

## KITABU CHA UFUNUO NA MNYAMA AMBAYE JERAHA LA KIFO LIMEPONA

**Somo Kuu: Daniel 7; pia Ufunuo 13:1-3.**
**Fungu La Kukariri: "Amebarikiwa anayesoma maneno ya unabii huu na wale wanaosikiliza na kuzingatia yale yaliyoandikwa humu, maana wakati umekaribia." Ufunuo 1:3.**



**Maelezo**. Itazingatiwa kwamba imani ni mojawapo ya karama maalum za Roho ambazo huja kama tokeo la vipawa viwili vilivyotangulia, vya hekima na maarifa.

6. Karama ya nne ya Roho Mtakatifu ni ipi? Mstari wa 9 (sehemu ya mwisho).
7. Zawadi zingine ni zipi? Kifungu cha 10.
8. Je, kila mtu katika mwili wa Masihi lazima awe na baadhi ya karama za Roho Mtakatifu! Mstari wa 11 (sehemu ya mwisho).

*******************************

**Somo la Machi 18, 2023 (Adar 25, 5783).**

## ISAYA, NABII WA INJILI

**Maelezo**. Isaya alitabiri katika siku za Uzia, Yathamu, Ahazi na Hezekia, au miaka ya 758 hadi 698 B.C. Unabii wake kuhusu Masihi ni wa kushangaza sana. Karne saba kabla ya Masihi, usahihi wa kutimia ni ushuhuda bora wa Biblia kuwa imeandikwa kwa pumzi za Elohim.

**Somo Kuu: Isaya 55.**
**Fungu La Kukariri: Isaya 66:20.**



10. Je, hili lilitimia? Mathayo 3:1-3; Yohana 1:19-23.
11. Nabii Isaya alisema nini kingempata Masihi? Isaya 53:7-9.
12. Je, hili lilitimizwa? Luka 18:31-33; Mathayo 27:29, 30, 41, 43.

   **Maelezo**. Kwa kweli unabii unaohusiana na kuzaliwa na kifo cha Yahshua umetimizwa kwa njia ya ajabu sana. Ndio, hata kwa herufi. Tunaweza kuwa na uhakika kwamba yametimia hata kwa herufi.

*******************************

**Somo la Januari 21, 2023 (Tevet 28, 5783).**

## UNABII WA DANIELI

**Somo Kuu: Danieli 9**
**Fungu La Kukariri: Danieli 9:22.**

1. Baada ya hekalu la Sulemani kuharibiwa, wana wa Israeli walichukuliwa mateka Babeli, lakini ni kwa muda gani walifaa kukaa huko? Yeremia 25: 10, 11.
2. Baada ya wao kukusanywa kutokana na mtawanyiko huu, ni nini ilifaa itendeke kwa Babeli? Yeremia 25: 12, 13.

   **Maelezo**: Ni ukweli unaojulikana, kulingana na maandiko na pia historia, kwamba Wayahudi

1. Ni kwa lengo gani na ni kwa nani Kitabu cha Ufunuo kilitolewa? Ufunuo 1:1.
2. Ni wapi ambapo mnyama amenakiliwa kwanza katika maandiko? Danieli 7:2, 7.
3. Je! Ni nini kinatokea mara moja baada ya muda uliotolewa kwa ajili ya wanyama hawa wanne kutawala? Mstari 9, 10.
4. Je, Danieli alifadhaika kuhusu ono hili, na alifanya nini? Mistari 15, 16.
5. Malaika alitoa habari gani? Mistari 17, 18.
6. Ni mnyama gani kati ya hawa wanyama wanne Danieli alipenda kujua habari zake? Mistari 19, 20.
7. Ni kwa muda gani mrefu Danieli alimuona huyo mnyama (chini ya mamlaka ya pembe ndogo) akifanya vita na Watakatifu? Mistari 21, 22.

   **Maelezo**: Kadiri nguvu ya mnyama wa nne itaendelea kuwa hapa na kutumia nguvu zake dhidi ya mabaki ya kweli ya watu sasa, na baadaye hadi wakati utakapofika hili tumiliki ufalme, kwa hakika kuna umuhimu mkubwa kujua huyo mnyama ni nani na yuko wapi. Ni dhidi ya huyu mnyama, basi, ujumbe wa mwisho wa onyo utapeanwa.

8. Malaika alimwambia Danieli kuwa huyo mnyama aliwakilisha nini, na pia hizo pembe zake kumi? Mistari 23, 24.



9. Jinsi gani hawa wanyama walinganishwa na wanyama wa Ufunuo? Ufunuo 13:1, 2.

   **Maelezo**: Hebu tuchunguze kuhusu huyu mnyama. Wanyama katika Danieli walikuwa simba, dubu, chui, na mnyama mwingine bila jina. Maelezo zaidi yanasema kuwa mnyama huyu wa Ufunuo alikuwa kama chui, na miguu ya dubu, na kinywa cha simba. Hivyo basi tuna wanyama hawa watatu wa Danieli ambao wanajumuisha kwenye huyu mnyama mmoja katika ufunuo. Lakini maelezo zaidi ni kwamba huyu mnyama wa Ufunuo pia alikuwa na vichwa saba na pembe kumi. Pia elewa ya kwamba hii ilikuwa idadi kamili ya vichwa na pembe zote za wanyama wa Danieli. Hivyo basi mnyama wa Ufunuo ni mwili kamili wa wote wale wanyama wanne. Pia utawala wa Kirumi, wa nne kutawala dunia, ulitawala sehemu zote ambazo zilitawaliwa na hawa wanyama wanne, hivyo basi ilikuwa mchanganyiko wa hao wote katika huyu mmoja.

10. Ni nini imesemwa zaidi (ukilinganisha Danieli na Ufunuo) kuhusu mnyama - kazi na nguvu ya kutesa na kiwango cha uwezo wake? Danieli 7:25 (sehemu ya mwisho) na pia Ufunuo 13:5-7.



walikusanywa tena Yerusalemu na hekalu lingine likajengwa mahali ambapo hekalu la Sulemani lilisimama.

3. Wakati Daniel alikuwa akiomba kwa ajili ya kurejeshwa kwa Israeli, ni nani ambaye alimtembelea? Danieli 9:20, 21.
4. Ni kwa kusudi gani Gabriel alimtembelea Danieli? Danieli 9:22, 23.
5. Ni kwa muda mgani uliopeanwa kwa watu wa Israeli ili wafanye upatanisho kwa ajili ya dhambi na kufanya maridhiano kwa ajili ya uovu? Danieli 9:24.
6. Kuhusu adhabu ya Israeli, ni muda gani siku moja iliwakilisha? Ezekieli 4:5, 6.

   **Maelezo**: Kama ilivyoteuliwa kwa Israeli, siku moja kwa mwaka mmoja, wakati wa vipindi hivi vya adhabu, kwa kimantiki na maandiko tutatumia kanuni hiyo kwa vipindi vya adhabu vitakavyofuata. Kwa hivyo kipindi hiki cha wiki 70 itakuwa 70 mara 7 au miaka 490, kwa sababu kuna siku saba katika wiki moja.

7. Gabriel alimpa Danieli hakikisho kwamba amri itatolewa kwenda kujenga Yerusalemu. Baada ya amri kutolewa, itakuwa kwa muda gani hata zamani zake Masihi? Danieli 9:25 [sehemu ya kwanza]



**Somo la Machi 11, 2023 (Adar 18, 5783).**

## KARAMA ZA KIROHO

**Somo Kuu: 1 Wakorintho 12.**
**Fungu La Kukariri: Mika 3:8.**

1. Je, ni mapenzi ya Elohim kwamba kanisa lake linapaswa kujua kuhusu karama maalum za Roho Mtakatifu? 1 Wakorintho 12:1.
2. Ni nini kilisemwa kuhusu tofauti za karama, na usimamizi wa Roho Mtakatifu? Mstari wa 4, 5.
3. Ni nini kilisemwa kuhusu utofauti wa utendaji kazi na udhihirisho wa Roho Mtakatifu? Mstari wa 6, 7.

   **Maelezo**. Udhihirisho wa Roho Mtakatifu unatolewa kwa faida ya kila mmoja, na ukweli kwamba Elohim habadiliki kamwe katika namna yake ya kushughulika na watu binafsi inathibitisha kwamba nguvu hii hiyo, ambayo ilifanya kazi wakati huo katika tofauti hizi za karama, bado inadhihirishwa kati ya wana wa Elohim.

4. Je! Karama za kwanza za Roho Mtakatifu ni zipi? Kifungu cha 8.
5. Je! Karama ya tatu ya Roho Mtakatifu ni ipi? Mstari wa 9 (sehemu ya kwanza); Warumi 10:17.